MKULIMA WA SEVIA

Nakala ya bure

APRILI - OKTOBA, 2018 #7

# Kuwa mkulima bora kuliko jirani yako

*Christina Msalato na Abigael Mlonga ni marafiki na wachuuzi kutoka kijiji cha Msalato (Dodoma). Wakulima wadogo wadogo kama hawa hulipa bei nzuri ya mazao. Viwango vya faida zao ni vidogo, kwa mfano bei ya kununua ikiwa ni TZS 800, bei ya kuuza ni TZS 1000.*

"Ni wakati gani bora kulima nyanya, ikiwa nataka kupata bei nzuri zaidi kwenye soko"? Ni nani atanunua mazao yangu? Ninawezaje kuboresha mazao yangu, ili kila mfanyabiashara awe anataka kununua mboga zangu? Haya ni maswali wakulima wanapaswa kujiuliza, kabla ya kuanza uzalishaji wa kilimo cha mboga.



Picha: Mseti Mwita

*Kazi ya Christina na Abigael hufanywa rahisi na wakulima ambao hutumia mbegu nzuri zaidi zinazohamasishwa na SEVIA. "Tunafurahia ubora wa aina hii ya nyanya (Victory F1) na wateja wetu wanapenda pia. Inafanya tuuze kwa urahisi".*

Wakulima wadogo wa mboga nchini Tanzania wanakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na kuzalisha kwa msimu, kupanda na kushuka kwa bei, miundombinu duni na ukosefu wa masoko mbadala ya kuuza bidhaa zao. Katika makala hii tunatoa ushauri juu ya nini kifanyike ili wakulima waongeze wigo mpana wa soko. Tunatoa taarifa kuhusu masoko mbali mbali ndani na nje ya nchi, lakini ujumbe wetu muhimu ni: **"Kuwa mkulima bora kuliko jirani yako."**

## Nyakati bora za kuvuna

Kuzingatia msimu ni muhimu ili kupata bei nzuri ya mazao; kwa hiyo mipango sahihi ni muhimu kwa kila mkulima. Mipango inahusisha mlolongo mzima wa uzalishaji, hivyo kabla ya kuanza uzalishaji wakulima wanapaswa kutafakari juu ya:

- Chagua aina bora za mbegu ambazo zinaweza kukabiliana na wadudu na magonjwa; aina hizi hutoa mavuno mengi, bora na yenye uwiano sawa, ambayo huvutia zaidi masoko. Aina bora ya mbegu inasaidia kupunguza gharama za uzalishaji.
- Chagua aina ya mbegu ambazo zina sifa maalumu: mfano aina fulani ya pilipili ni kali zaidi kuliko nyingine; nyingine zina maumbo tofauti au rangi. Tofauti hizi zote zinaweza kuvutia wafanyabiashara fulani na kukupa faida ya kiushindani. Zingatia kulima mazao tofauti na yaliyozoeleka, ili kujitofautisha na wakulima wengine. Ukiwa mkulima mmoja wa bilinganya miongoni mwa washindani wachache unaweza kuwa na faida kuliko kuwa mmoja kati ya wazalishaji maelfu wa nyanya. Hakikisha kuna mnunuzi anayevutiwa na bidhaa yako.

- Kuwa makini: Soko halitabiriki. Bei za juu katika msimu mmoja zinaweza zisiendelee. Kinyume chake ... baada ya msimu mzuri wenye bei za juu wakulima wengi hudhani msimu ujao utakuwa sawa na wote hulima zao fulani. Kisha soko hufurika na bei hushuka.
- Lenga mavuno nje ya msimu ikiwa kuna upatikanaji wa maji ya kutosha. Wakulima wengi hupanda mboga msimu wa masika (Machi hadi Julai). Kwa sababu ya uhaba wa maji ya umwagiliaji, wakulima wengi hujiepusha na kilimo cha mboga wakati wa vuli/ukame (Agosti hadi Februari). Bila shaka hii ina athari katika upatikanaji na tofauti ya bei: kwa ujumla bei ya mboga kama nyanya, vitunguu, pilipili hoho, kabichi na tango ipo chini kuanzia Juni hadi Desemba na hupanda kuanzia Januari hadi Mei.


Picha: Elijah Mwashayenyi

Latifa kutoka SEVIA anaonesha aina ya bidhaa ambayo iko tayari kwa soko

Maarifa ni muhimu: wakulima wanapaswa kujua nini wanataka na kupata ujuzi katika kila hatua ya uzalishaji wa mboga. Mfano: wakati wa kuanza kusia mbegu kipindi cha mvua fupi na kiasi cha maji kinachohitajika, namna ya kuhifadhi au kufungasha mboga hadi uuzaji. SEVIA ipo kwa ajili ya kutoa ushauri. Ushirika wa wazalishaji matunda na mazao ya bustani Tanzania (TAHA) hutoa bei za mazao katika masoko mbalimbali na mwenendo wa bei za mbogamboga.

## Wapi pa kuuza mazao?

Utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na SEVIA na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi ulionesha kuwa ingawa kuna masoko ya nje katika nchi za Mashariki ya Kati, Ulaya na mahali pengine, wakulima wadogo nchini Tanzania hawana uwezo wa kufikia masoko haya, ambayo hufikiwa na wafanyabiashara wakubwa.


Picha: Franco Kajuna

Elius Amos wa Buhila (Mwanza) anauza mazao yake kwa urahisi, kwa sababu mavuno ni bora

Kwa bahati mbaya maduka makubwa kama Shoprite, Uchumi na Nakumatt yamefungwa kutokana na masuala ya ndani ya kitaasisi na mahitaji madogo ya bidhaa kwa walaji. Hivyo wakulima wadogo watakutana na wanunuzi kwenye masoko ya wazi na watalazimika kuendelea kuwazalishia mboga bora. Kuna masoko mengi ya wazi Tanzania, kuanzia


Picha: Mseti Mwita

Hakuna tatizo kwa Richard Augustino (Dodoma): wateja watamtafuta!

ngazi ya kijiji hadi masoko ya miji mikubwa. Masoko mengine ya kijiji huuza bidhaa kwenye siku zilizochaguliwa, mara moja au mara mbili kwa wiki. Hata hivyo, masoko makubwa hufanya kazi kila siku. Baadhi ya masoko makubwa ya wazi ni:

| Mkoa | Mahali |
|---|---|
| Kilimanjaro | Mbuyuni– Moshi<br>Sadala (Hai)<br>Soko la kati |
| Mtwara | Soko kuu |
| Lindi | Soko kuu |
| Zanzibar | Soko kuu<br>Darajani<br>Forodhani |
| Mbeya | Soweto<br>Sido<br>Tukuyu - Ushirika |
| Morogoro | Soko kuu<br>Gairo - Kilosa |
| Iringa | Soko kuu<br>Ilula |
| Arusha | Kilombero (Mjini)<br>Tengeru Meru)<br>Namanga (Mpakani Tanzania- Kenya) |
| Mwanza | Soko kuu (Mjini)<br>Kirumba (Ilemela)<br>Buhongwa |
| Dar es Salaam | Kariakoo<br>Temeke<br>Mabibo<br>Kisutu<br>Shekilango<br>Sinza |

## Na pia wasindikaji...

Usindikaji wa mboga unazidi kushamiri katika baadhi ya maeneo na unaongeza fursa zaidi kwa wakulima. Wasindikaji katika nyanda za juu kusini kama Redgold, Dabaga na IVORI wanapatikana Iringa wakati Marriet Natural Foods anapatikana Njombe. Darsh Industries Limited kutoka Arusha ni msindikaji anayeongoza kwa bidhaa za matunda na mboga na pia ni msindikaji mkubwa wa nyanya nchini. Serengeti Fresh (Arusha) ni mkulima, msindikaji na anasafirisha nje na huingia mkataba na wakulima wadogo ili walime mazao, kama maharage machanga. Sekta ndogo za usindikaji wa mboga mboga kama chachandu na ketchups zinazidi kujiendeleza katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Zanzibar, Arusha na Mwanza. Wakulima wadogo wanaweza kuongea na makampuni haya kama watapenda

**SEVIA na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi** walifanya utafiti katika miji mikubwa na midogo iliyochaguliwa ikiwemo Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Iringa, Morogoro, Mbeya, Zanzibar, Lindi, Mtwara na Moshi. Jumla ya washiriki 131 waliojumuisha wakulima, wafanyabiashara, wasindikaji, mameneja wa maduka makubwa na mmoja wa wasafirishaji bidhaa nje walidodoswa.

**Baadhi ya hoja za kweli kutokana na uchambuzi:** Kwa watu waliohojiwa, 72% ya wafanyabiashara walikuwa wanawake. Hii ni kutokana na sababu kuwa biashara inahitaji mtaji mdogo na inafanywa hasa katika maeneo ya karibu. Hii huwapa wanawake muda zaidi kutunza familia zao. Wakulima wengi takribani (97%) huuza mazao kwa bei ya jumla kwa wafanyabiashara ili kupata muda wa kufanya shughuli nyingine na kupunguza gharama za kuuza mazao hayo. Wakulima wachache tu (3%) hupendelea kuuza kwa rejareja, na hata hivyo ni siku za soko tu kwa masoko ya karibu.

# HABARI KUTOKA SHAMBANI

## ISHI MAISHA HURU YA KUJITEGEMEA



Picha: Elijah Mwashayenyi

Joseph Burton kwenye shamba lake la nyanya

**Joseph Burton (miaka 24) kutoka Lusungo (Mbeya) analima nyanya, chainizi kabichi, pilipili kali, vitunguu, pilipili hoho na mahindi tangu mwaka 2012. AliIfahamu SEVIA kupitia mafunzo ya wakulima yaliyoongozwa na Frank Mazengo wa SEVIA kwenye shamba darasa la jirani.**

Kupata mavuno machache na muda mfupi wa nyanya kukaa shambani ilikuwa ni changamoto kubwa. Kupitia SEVIA, alijifunza matumizi sahihi ya mbolea na kufungia mazao. Baada ya kutimiza hayo alipata matokeo mazuri, ikiwa ni pamoja na mimea kukaa kwa muda mrefu shambani. "Takribani nimepata mara mbili ya mavuno yangu", alisema. "Baada ya misimu mitatu mfululizo niliweza kuanzisha familia na kufungua duka la rejareja. Sasa ninaishi maisha huru ya kujitegemea."

## MAFANIKIO YA UPATIKANAJI RAHISI WA SOKO



Picha: Nurdin Mndoholele

Wakulima walioungana wanafuraha kuona mavuno yao

**Amos Kimilomilo (28) na Iddi Mahamudu (29) ni wakulima wadogo kutoka Budebude (Bagamoyo). Tangu mwaka 2016 waliungana na kufanya kilimo cha bamia, nyanya chungu, nyanya, pilipili hoho na mahindi. Sasa wanajihusisha zaidi na nyanya na pilipili hoho.**

Msimu uliopita walipata shida kuuza kreti 28 za nyanya za kienyeji kutokana na ubora duni wa mazao. Walikutana na Nurdin Mndoholele (afisa ugani wa SEVIA) na kufuata ushauri wake, walitumia mbegu chotara, matumizi sahihi na salama ya mbolea, viuatilifu na kufungia mazao. Hadi sasa wameuza kwa urahisi kreti 20 aina ya Gahmar F1 kwa wiki mbili walizovuna kwenye eneo lilelile la ukubwa wa 250m$^2$. Wanatarajia kuvuna kwa wiki tatu zaidi na kupata mara mbili ya mavuno ya awali. Hata hivyo, kutokana na ubora wake hawatakuwa na shida ya kuuza mazao yao.

Wakulima hawa wamepanga kuwa na miche 2000 ya nyanya (Gahmar F1) na 3000 ya pilipili hoho (Mekong F1) katika msimu ujao.

"Tulichelewa kupata ujuzi huu. Huenda tungekuwa mbali sana sasa", walicheka. "Hata hivyo, tunaangalia mbele kwa tumaini kubwa kwa sababu tumepewa uwezo wa kufikia mafanikio."

## SASA NIMEJIAJIRI MWENYEWE



Picha: Mseti Mwita

Eugene Sanga akifungia tango (Mydas F1) ndani ya nyumba kitalu yake ya mbao

**Eugene Senga (33) kutoka Mbwanga (Dodoma) ni mkulima wa nyanya, pilipili hoho na nyanya chungu kwa miaka 6 sasa. Mwaka 2017 alishiriki katika ujenzi wa nyumba kitalu kwenye uwanja wa Nanenane huko Dodoma chini ya mtaalamu wa SEVIA George Kisamo. Mbali na hapo alipata ujuzi kuhusu uangalizi wa mazao wakati akifanya kazi na afisa ugani wa SEVIA Mseti Mwita.**

"Sasa nimejenga nyumba kitalu yangu ya mbao na nilipata kazi ya TZS 600,000 kwa mkulima wa Rorya kwa ajili ya kujenga nyumba kitalu nyingine. Sikujua kamwe kama ningeweza kujiajiri kwa njia hii kwa jinsi wakulima wanavyotaka niwajengee nyumba kitalu," alisema Eugene.

Eugene pia alijifunza umuhimu wakutumia mbegu chotara kwa kilimo cha nje na kwa kutumia mbegu hizi na mbinu bora za kilimo alipata mavuno mengi. Kwenye eneo la ardhi la ukubwa wa 300 m$^2$, alipata kreti 52 za nyanya ambazo huwezi kulinganisha na kreti 27 alizopata kabla kwa kutumia mbegu za kienyeji.

"Hakuna nachoweza kuilipa SEVIA zaidi ya kufundisha wakulima wengine matumizi ya mbegu chotara katika uzalishaji wa nyumba kitalu", alisema

# VIDOKEZO

## Fahamu njia za asili za kudhibiti wadudu sumbufu na magonjwa

**Uzalishaji wa mboga mara nyingi unahusisha matumizi ya viuatilifu vyenye kemikali. Wakulima baadhi hawawezi kumudu gharama kubwa za viuatilifu hivi, ambavyo visipotumika vizuri huweza kuleta madhara, kama kuharibu mazingira, mimea na kuathiri watumiaji wa mboga. SEVIA pia inahamasisha njia za asili katika kupambana na wadudu sumbufu na magonjwa bila kemikali.**




Bamia iliyozalishwa bila kemikali katika kanisa la katoliki Mailisita, wilaya ya Hai

### Uchaguzi wa mbegu bora na kukuza miche yenye afya husaidia kudhibiti wadudu / magonjwa

Mimea yenye afya na nguvu inaweza kustahimili mashambulizi ya wadudu na magonjwa. Chagua mbegu zinazoweza kuvumilia wadudu na magonjwa na kuza miche yako kwenye trei/viriba au kitalu cha ardhini kilichoboreshwa kwa kutumia udongo uliotibiwa kwa kuoteshea. Unapoanza na miche yenye afya utapunguza matumizi ya viuatilifu na gharama zako za uzalishaji.

### Njia za asili za udhibiti wa wadudu zinazopendekezwa

Kumbuka, sio wadudu wote wanakula mazao yako, baadhi husaidia kupunguza wadudu wengine kwa kiasi kinachotakiwa. Wadudu 'wazuri' hujumuisha nyigu, vunjajungu, kombamwiko na mbawafungo ambao wanakula wadudu wengine.

## Unajua kwamba...

### Usafi wa shamba ni muhimu

Msimu wa mvua nyingi ni kipindi ambacho magugu mengi huota shambani na hutumika kama maficho ya visumbufu vya mazao. Wakati wote hakikisha shamba lako halina magugu. Mimea yenye magonjwa ing'olewe na kutupwa kwa utaratibu mzuri, ikiwezekana kufukiwa au kuchomwa mbali na shamba. Ondoa mabaki yote baada ya mavuno kwani vimelea vya magonjwa na wadudu hubaki kwenye mabaki hayo.

Kombamwiko hula vimamba






Mche uliyowekewa majivu kuzunguka kitako cha shina

Uharibifu wa sota/funza mkataji unaweza kuzuiwa kwa kuweka kizuizi kuzunguka mimea au kupaka majivu juu ya kitako cha mmea. Vile vile wanaweza kufukuzwa kwa kuweka shina la kitunguu kuzunguka shina la mche.

Jamii ya konokono wanaweza kuwa wavamizi wabaya pia. Unaweza kuwafanyia ujanja kuwakamata: Wakati wa alasiri laza chini kipande kipana cha mbao karibu na mimea inayoota; konokono na jamii yake hupenda kujificha na kula. Asubuhi inayofuata unaweza kuwakusanya kutoka chini ya ubao na kuwaangamiza.




Majani ya mwarobaini

Kwa ujumla ni rahisi sana kwa aina ya visumbufu wakubwa kwani unaweza kuwaokota na kuwaua, mfano viwavi

## Viautilifu vya kibaolojia/asili

Majani ya mwarobaini ni kiuatilifu cha asili chenye uwezo wa kudhibiti wadudu kama vimamba, mbawakawa/kombamwiko, panzi, Funza/viwavi, mbawakawa wa kijapani, nzige, wadudu wenye magamba laini, chawa/vithiripi, fukusi, utitiri na nzi weupe.

Majani ya basili/mfumbasi yanaweza kuwa suluhisho mbadala katika kudhibiti viwavi, nzi wa matunda, utitiri wekundu, utitiri weupe, wadudu wenye magamba laini, kombamwiko wa madoa, magonjwa ya fangasi na minyoo fundo.

Kwa kutumia vitunguu swaumu unaweza kudhibiti viwavi, nzi wa matunda, utitiri wekundu, utitiri weupe,wadudu wenye magamba laini, kombamwiko wa madoa, magonjwa ya fangasi na minyoo fundo. Mchanganyiko tajwa hapo juu unaweza kutumiwa kudhibiti wadudu wanaofyonza na kutafuna. Mchaichai ni bora kwa kuzuia bakajani/ukungu na magonjwa ya bakteria katika mboga

**Tafadhali angalia tovuti ya sevia kufahamu jinsi ya kuandaa viuatilifu hivi au uliza afisa ugani wa Sevia wa eneo lako kwa taarifa zaidi.**

# Maonesho maalumu ya shamba darasa Wilaya ya Babati, wakulima 109 wahudhuria

**Kiasi kikubwa cha watu 109 walihudhuria maonesho maalumu ya shamba darasa huko Babati yaliyolenga umuhimu wa mbolea yenye kirutubisho cha potasiamu kwa ukuaji wa nyanya na kutambulisha aina mpya ya nyanya, Gahmar F1. Tukio hilo, lilishirikisha moja ya washirika wa SEVIA, Rijk Zwaan, ikiwa ni onesho la 7 (kati ya maonesho 26 ya shamba darasa msimu wa mazao wa Okt 2017 – Febr 2018) yaliyoandaliwa na SEVIA.**



Picha: Janeth Mollel

Bw Rashid Malomba Barie anawasaidizi wa kutosha katika mradi wake wa kilimo

Maonesho haya yalifanyika kijiji cha Ayasanda kwenye shambaa la Rashid Malomba Barie, mkulima mkongwe mwenye umri wa miaka 79 ambaye bado anaweza ushindani. Tukio hili lilikuwa na maafisa 5 wa serikali ikiwa ni pamoja na Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika Wilaya (DAICO) Bi Jetrida Kyekaka. Mkurugenzi Mtendaji wa SEVIA, Elijah Mwashayenyi alizungumzia umuhimu wa kutafuta masoko na kutumia mbegu bora pamoja na mbinu bora za kilimo. "Wakulima wanapaswa kuongoza katika kutafuta masoko", alisisitiza Meneja ugani Epaphras Milambwe. Mathhew Ngoma (Rijk Zwaan) alielezea faida za kutumia mbegu bora ikiwa ni pamoja na mbegu ya nyanya kutoka Rijk Zwaan Gahmar F1 na Jarrah F1.
Bi Kyekaka katika kuongea kwake aliwaomba Rijk Zwaan wafungue tawi Babati ili kufanya mbegu zao zipatikane kwa urahisi. Mwenyekiti wa kijiji Elias Bombo aliishukuru SEVIA kwa kuchagua Babati kama moja ya wilaya zake za kazi na akaomba Babati iwekwe kwenye ramani ya uzalishaji wa mboga.



Picha: Janeth Mollel

Afisa ugani wa SEVIA Ladislaus Mkufya akielezea malengo ya shamba darasa

Wakulima wawili vijana, Erasto Elias ambaye amekuwa akijifunza kutoka kwa shamba darasa la Bw Malomba na Abubakari Saidi kutoka Kikore-Kondoa, walitoa shuhuda kuhusu ushirikiano wao na SEVIA ulivyobadilisha maisha yao. Mkulima mwenyeji Rashid Malomba hakuweza kuficha furaha yake kwa kilichomshangaza: "Napenda kuwashukuru SEVIA na afisa ugani wao Ladislaus Mkufya. Ni kijana mwenye bidii ambaye unaweza kumpigia wakati wowote. Amenielekeza kutumia mbegu bora na matumizi sahihi ya mbolea, naweza kupata mazao mengi katika eneo dogo. Kwa wakulima wenzangu ninasema, ikiwa naweza kuzalisha kiasi hiki kwa umri wangu, wote mnaweza kufanya hivyo ● "

Gahmar F1, mbegu bora mpya mjini. Watu wote waliohudhuria walishangaa kiasi cha matunda kilichobebwa na zao hili la nyanya. Mkulima mmoja alitikisa kichwa akasema "Sijawahi kuona kitu kama hiki."



Picha: Janeth Mollel

# MAONESHO YA SHAMBA DARASA YA SEVIA: MFUMO WA KUPEANA TAARIFA NA KUNDI KUBWA LA WATU



Picha: Halima Jumanne

Kuanzia Januarai 2018 hadi Machi 2018, SEVIA na wakulima wamefanikisha jumla ya maonesho ya shamba darasa 26. Maudhui ikiwa ni pamoja na utunzaji wa kitalu, matumizi sahihi ya mbolea, udhibiti wa visumbufu zao na magonjwa, kufungia mazao yanayotambaa, matumizi ya mbegu chotara dhidi ya mbegu za kawaida na kupogolea. Mazao yaliyozungumziwa hasa ni nyanya, tango na pilipili hoho. Mahudhurio yalikuwa kati ya wakulima 14 kwa kiwango cha chini hadi wakulima 119 kwa kiwango cha juu. SEVIA imefikia zaidi ya wakulima 1300 kupitia maonesho haya ya shamba darasa.

Maonesho ya shamba darasa ya SEVIA hufanyika kwenye kilele cha msimu; wakati mazao yamekomaa na mavuno yanakaribia. Hii ni hatua ambayo tofauti zilizosababishwa na teknolojia bora, mbinu bora na aina bora ya mbegu huonekana kwa wote na wakulima wenye mashamba darasa hutoa shuhuda juu ya faida za teknolojia hizo. Hivyo maonesho haya ni jukwaa la kushirikishana taarifa juu ya mbinu bora ambazo zitaboresha uzalishaji, tija na masoko.

Kwa kawaida maonesho ya shamba darasa ya SEVIA huanza na usajili wa wakulima na washiriki wengine. Kisha washiriki huelezwa kusudi la maonesho na utaratibu wa siku hiyo. Hii hufuatiwa na ziara shamba ili kuona matokeo ya ufanisi wa teknolojia mbalimbali; "Kuona ni kuamini". Baadae; hufuata kipindi cha maswali na majibu kinachoongozwa na maafisa ugani wa SEVIA. Hiki ndiyo kipengele muhimu na huchukua muda mwingi. Mkulima mwenyeji na wakulima wengine hupata fursa ya kushirikishana uzoefu wao na mbinu bora zilizooneshwa. Maonesho haya huhitimishwa kwa nasaha kutoka kwa kiongozi wa serikali ya mtaa au mtaalamu wa kilimo.

*Kwa **maonesho maalumu** ya shamba darasa, angalia mfano kutoka Babati kwenye ukurasa uliopita.*



# KONA YA TAFITI

## Mapendekezo ya mbolea ya samadi

SEVIA hivi karibuni ilifanya jaribio la kutumia mbolea ya samadi (yenye 1.5% ya nitrojeni) katika uzalishaji wa kabichi. Matokeo yameleta mapendekezo yafuatayo:

- **Ikiwa kilo zitatumika: Itahitajika kilo 12,000 (au tani 12) kwa ekari**
- **Ikiwa ndoo ya lita 20 (inayokadiriwa kubeba kilo 10 za samadi) itatumiwa: Itahitajika ndoo 1200 kwa ekari**
- **Ikiwa toroli (linalokadiriwa kubeba kilo 50 za mbolea) litatumiwa: Itahitajika toroli 240 kwa ekari**
- **Ikiwa mkokoteni wa punda (unaokadiriwa kubeba toroli 10) utatumiwais: Itahitajika mikokoteni 24 kwa ekari**

# AJENDA

| MACHI | APRILI | MEI | JUNI | JULAI | AGOSTI |
|---|---|---|---|---|---|
| Mafunzo kwa wakulima... | | | | | |
| | | Mafunzo kwa wataalamu | Mkutano mkuu wa bodi | Maonesho ya shamba darasa ya SEVIA | Maonesho ya Nanenane |


## WACHANGIAJI

MKULIMA WA SEVIA

**Anuani ya posta**
SEVIA, P.O. Box 7211, Moshi

**Anuani ya kutembelea**
Lambo, Mferejini
Tanzania
+255 685 942 364
www.sevia.biz

**Michango ya jarida hili ni kutoka kwa**
- Halima Jumanne
- Epaphras Milambwe
- Elijah Mwashayenyi
- Herman de Putter
- Anita van Stel
- Frank Mazengo
- Nurdin Mndoholele
- Mseti Mwita
- Flip van Koesveld

SEVIA • Wageningen UR • Communications consultant

**Wahariri**
Halima Jumanne
Elijah Mwashayenyi
Anita van Stel

**Ubunifu**
Mooizo Design

WAGENINGEN UNIVERSITY & RESEARCH

**Je, unataka kupokea nakala za bure za awali za jarida hili? Tafadhali tuma barua pepe au soma jarida katika tovuti yetu www.sevia.biz**